

Jina.....
Shule.....

Nambari.....
Sahihi.....
Tarehe.....

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI/ AGOSTI
Muda : 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO YA KCSE WA WILAYA YA KERICHO

Hati ya kuhitimu masomo ya sekondari (K.C.S.E 2012)

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI/ AGOSTI
Muda : 2 ½

Maagizo.

1. Andika jina na nambari yako katika nafasi uliyoachiwa.
2. Jibu maswali yote .
3. Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki.
4. Hakikisha karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya mtihani.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

*Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu naswali

Haki za watoto na wanawake

Makamishina wa Tume za Haki za Binadamu, waandalizi, waalikwa, watoto, mabibi na mabwana. Kwa muda mrefu kumekuwa na tofauti katika uhusiano baina ya wanajamii. Tofauti hizi zimewapelekea wanawake na watoto kudunishwa. Uduishaji unachukua mwelekeo mbaya zaidi kama watoto ni wa kike.

Kupuuzwa kwa wanawake na watoto kuna historia ndefu. Jambo hili limepata **usugu** kutokana na imani hasi **zilizoota akilini** mwa wanaume na hata wanawake. **Rasilimali** na majukumu yamegawanywa kwa misingi inayowatabakisha wanajamii kuanzia wanaume, wanawake halafu chini kabisa watoto. Katika jamii yingi, wanawake na watoto wa kike hawarithi, chochote ingawa ndio wenyewe mchango mkubwa katika uzalishaji mali. Aidha mchango wao kuhusu masuala muhimu nyumbani na katika jamii hupuzwa hate kama wamesoma kutiko waume na akina baba zao.

Inasikitish7a kuwa wanawake na watoto hawana sauti kuhusu uamuzi nyumbani. Wao hulazimishwa kutenda wanavyoamriwa na wanaume. Kwa mfano, si ajabu mwanamke kulazimishwe kupika pombe na watoto kusukumizwa kwenda kununua sigara. Yote haya ni kinyume cha matarajio ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu.

Ili kuzuia tabia ya ‘ujuaji’, wanaume wengi hupiga marufuku redio, simu, magazeti na televisheni kwa wanawake na watoto. Amri hii hutekelezwa vikali ill wahusika wasijifunze tabia ye **kukaidi amri** za wazee. Pengine hii ndiyo sababu katika jamii fulani, neno mzee lina maana moja tu; ya wanaume waliokomaa kiumri wale si wenawake. Hii si kweli.

Haki za binadamu ni msingi we utu. Bila haki hizo mwanadamu hawezi kutumia vipawa na uwezo wake wa kiakili na kihisia kikamilifu. Uduishaji wa wanawake na watoto unapingana na ukweli huu. Imani potofu zinazoendeleza uovu huu zimejikita akilini na katika utamaduni. Zinahitaji kuondolewa. Nafurahi kuwa **mmeibua** mikakati thabiti ya kulipiga vita tatizo hili. Kwa kweli, sherehe kama hizi ni muhimu sana katika kuwafumbua macho wadau kuhusu haki za wanawake na watoto. Naamini hotuba zilizotolewa hapa zitakuwa mbegu zitakazochipua mabadiliko katika fikra na matendo ye watu. Yafaa watu wakubali kuwa mke na watoto ni wenza na wadau katika safari ndefu ye maisha.

Nimeona mabango, maigizo, ngoma na michoro ya waume kwa wake, wazee kwa watoto na wavulana kwa wasichana kuhusu made hii. Ujumbe umewasilishwa wazi. Ni **moyo uliofumwa kwa chuma** tu ambao hauwezi kuathiriwa na ujunibe kuhusu nafasi ya wanawake kurithi na kusikilizwa. Lakini vita vya panga haviamuliwi kwa fimbo. Kilichobaki sasa ni kufanya utatiti wa kukusanya data kuhusu mielekeo © 2012 Kamati ya Elimu ya Wilaya ya Kericho 2 Kiswahili 102/2 Fungua kurasa

na itikadi zinazopingana na lengo letu. Kutokana na matokeo, mikakati iwekwe ili kuvunja nguvu, desturi zinazochochea taasubi za kiume.

Mabibi na mabwana, yapasa juhudini zifanywe za kusambaza habari kuhusu umuhimu wa kuheshimu na kujali binadamu wote na mchango wao. Aidha hatuna budi kuhakikisha nafasi sawa kwa kite mtu kutoa maoni na kusikizwa. Litakuwa jambo la kusikitisha kama jamii itasahau mchango wa wanawake na watoto katika kuzalisha na Kulinda mali. Twahitaji kuondoa uoga kutoka kwa mama zetu wasiotaka mabadiliko. Sekta zote za umma lazima zijitahidi kutekeleza haya.

Ningependa kwakumbusha kuwa kanuni za ubalozi hazziniruhusu kuingilia masuala ya ndani ya nchi hii. Hata hiyo, nalazimike kushauri jambo moja. Nashauri ibuniwe Wizara ya Maendeleo ya Wenawake, Vijana na Watoto. Wizare hii itakuwa na jukumu Ia kuondoa vikwazo dhidi ya wanyonge.

Kubuni wizara tu hakutasa idia. Wakereketwa washawishi mabadiliko katika sheria kuhusu wanawake na watoto hasa wajane na mayatima. **Wanaharakati** nao yapasa wahakikishe kuwa sheria hizo zinaheshimiwa. Shirika langu liko tayari kutoa msaada wa kifedha na kitaaluma kwa sababu hii.

Mambo haya yasikomee hapa. Mrudi mlikotoka na mbuni vikundi vya kutuutilia mapendekezo yaliyotolewa. Ni muhimu kusambaza mliyojifunza hapa ili mambo hayo yapenye kila nyumba. Asanteni.

- (a) Tambua na kuthibitisha anayehutubia washika dau. (al.2)

.....
.....

- (b) Eleza mielekeo hasi inayopeleka wanawake na wanaume hudunishwa. (al.4)

.....
.....
.....
.....

- (c) Kwa kuzingatia swala ibuka la haki, orodhesha haki zozote tatu ambazo wanaume na watoto wananyimwa (al.3)

.....
.....
.....
.....

- (d) “Vita vya panzi haviamuliwi kwa fimbao” (al.2)
Fafanua

- (e) Taja mchango wa mwandishi wa hotuba hii katika kuirekebisha hali hii ya kudumisha wanawake na watoto. (al.2)

- (f) Eleza maana ya
(i) Kukaidi amri

- (ii) Moyo uliofumwa kwa chuma

2. UFUPISHO

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi Ia dhana ya “ujambazi” tena “Wa kimataifa”. Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi wa nchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambazi ni balaa kweli, tena belua, lakin huo ni wa huko, wala hauwezi kuwashtua licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni ya watakaburi hao, ujambazi ni wa watu ‘washenzi’ wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi pekee wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevyta uliosabäbishwa na vinyangarika kutoka nchi hizo maaluni za “ulimwengu wa tatu”. Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusagwasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka va 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako!

Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba

ingewezekana taifa lolote au mtu ye yeyote kuthubutu kuishambulia nchi yao, taifa wasifa lili lojihami barabara dhidi ya aina yoyote lie ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima paliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kushereheke. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha ya Newyork na lile la Pentagon, qti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ilizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kwa ni majambazi wa kimataifa.

MASWALI

Bila kubadilisha maana,fupisha aya tatu za kwanza maneno (65-75) (alama 8; 2 za utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

- (b) Ukizingatia aya tatu za mwisho fafanu fikra za watu n amambo yote yaliyotokea baada ya Septemba 11 2001(Maneno 65/75) Alama 7:alama 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

3. **Matumizi ya lugha (alama 40)**

- (a) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo:

Mwanamke huyo alibebwa juu juu hadi kanisani.

(al.2)

- (b) Bainisha jinsi mahenoyaliyopigiwa mstari yalivytumika.

(al.2)

(i) Kula kwake ni chanzo cha afya yake nzuri.

(ii) “Kula vizuri kama unataka kuwa na afya bora”. Daktari alisema.

- (c) Sauti /e/ na /u/ hutamkwa vipi?

(al.2)

- (d) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii

(al.2)

Mvua iliyonyesha jana ilisababisha madhara makubwa.

- (e) Andika mifano mitatu tofauti ya Nomino katika ngeli ya U-ZI.

(al.3)

- (f) Tumia kirejeshi ‘O’ tamati katika sentesi ifuatayo :

Kalamu ambayo alinunua ni ile ambayo anaipenda

- (g) Tambua yambwa tenda na yambwa tendewa katika sentesi ifuatayo.

Maria alimnywesha mtoto maziwa jana asubuhi.

(al.2)

(h) Tumia viakifishi vifuatavyo kutunguu sentensi sahihi (al.2)

(i) Kibainishi

(ii) Mstari

(i) Unda nominō kutokana na vitenzi vifuatavyo (al.2)

(i) Nasihi

(ii) Arifa

(j) Tunga sentensi ukiyatuma maneno haya. (al.2)

(i) Mjusi

(ii) Mali

(k) Eleza matumizi ya viambishi vilivyopigiwa kistari. (al.2)

(i) Kaketi

(ii) Nikisoma kwa bidii nitapita mtihani

(l) Tunga sentensi mbili ukitumia ‘a’ - unganifu pamja na maneno yafuatayo (al.2)

(i) Uaminifu

(ii) Ng’ombe

- (m) Tunga sentesi ukitumia kihisishi kifuatacho
Kefule (al.1)

- (n) Bainisha aina za viterzi katika sentensi hizi (al.2)
(i) Wewe u mwananchi wa Amerika

- (i) Jana nilinunua mkate na maziwa (al.2)

- (o) Yakinisha sentensi hii katika nafasi ya pili umoja.
Tusipolewana na walimu hatutapata amani siku zote shulen

- (p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (al.5)
Gari nene jeupe lililoibwa Kisumu limepatikana Nairobi.

(q) Tunga sentensi kubainisha maana ya vitate hivi. (al.2)

Gaidi

.....

Kaidi

.....

(r) Geuza sentensi ifuatayo liwe kwa udogo

Shule hiyo msichana anayeshiriki katika riadha. (al.2)

.....

(s) Andika upya sentensi kwa kufuata maagizo. (al.1)

Anaimba vizuri na anawavutia mashabiki wengi

Anza kuimba

.....

4. Isimu jamii

Eleza tano sababu zinazofanya kilugha ~~sheng~~^{shar} kutoteulina kama lugha ya taifa.

(al.10)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com